

## Taasubi katika Shirikana za Kivumba: Mtazamo wa Kisemiotiki

Sanja, L. W. Leo  
*Chuo Kikuu cha Nairobi*

### Ikisiri

Makala haya yanachunguza baadhi ya shirikina za Kivumba kwa nia ya kubainisha ya kwamba, zinaashiria kuwepo kwa taasubi ya kiume katika jamii husika. Hakuna usawa wa kijinsia katika masuala kama vile malezi ya watoto na ulaji wa vyakula hasa kwa mwanamke. Ili kukuza mjadala wetu, makala yamefafanua ishara na maana kama zinavyojidhihirisha katika baadhi ya mifano ya shirikina za Kivumba. Makala haya yanachukulia kwamba sio rahisi kufasiri ishara na maana katika shirikina za jamii yoyote nje ya mkutadha wa jamii hiyo. Ushahidi wote unaotegemewa katika mjadala wetu ulitokana na mifano iliyokusanywa kutoka nyanjani.

**Maneno Muhimu:** shirikina, kivumba, semiotiki, taasubi, ishara

### Utangulizi na Mapitio ya Maandishi

Hadi sasa, hakuna utafiti wa kinadharia kuhusu fasihi simulizi ya Kivumba kuhusu shirikina. Shirikina na utamaduni hufungamana na huathiri namna wanajamii hufasiri ulimwengu wao (Senkoro, 2012). Maadili na amali za jamii hutegemea mikatale ambayo huielekeza jamii na kuistiri dhidi ya matendo ijapo kilimwengu huenda yasionekane kuwa na kasoro lakini kwa wenyeji yana athari kubwa. Dhima yake kuu ya shirikina ni kuzawazisha urazini miongoni mwa wanajamii na kuzuia ukengeushi unaotokana na mtagusano na mazingira ya nje ya utamaduni husika. Shirikina katika jamii ya Kivumba zinaathiri sekta zote za maisha ya Kivumba na kila mwanajamii anatarajiwa kuziheshimu (Sanja, 2019).

Wamitila (2003) na Wellek na Warren (1949) wanabainisha ya kwamba, ingawa fasihi ni kazi ya kubuni, huashiria ukweli kwa njia ya kutumia ishara za lugha kwa ubunifu ili kumulika masuala ya kijamii kwa inayoathiri na kushawishi. Kama anavyosema Leech (1969), fasihi hutumia lugha ya kitamathali ambayo huwa na ishara nyingi. Shirikina kwa kiwango kikubwa hutumia ishara mbalimbali kuashiria maana mbalimbali. Namna wanajamii hufasiri maana kutokana na ishara husika hutokana na mazoea na tajriba ya jamii husika ya muda mrefu (Wamitila, 2003). Kwa mujibu wa Mbatia (2000) anasema ya kwamba, wanajamii wengi hujibainisha kama wasioamini katika imani za kishirikina wanapokuwa nje ya jamii na tamaduni zao. Hata hivyo, wanapokuwa katika mazingira ambamo shirikina husika zinachipukia, wao huzimini kikamilifu. Malighafi makuu ya fasihi

simulizi ni jamii (Senkoro, 1982). Senkoro anaelekea kujadili kuwa, sio rahisi kufasiri ishara na maana ya shirikina nje ya muktadha wa jamii husika. Kila jamii ina namna yake ya kufasiri ishara zinazotumika katika matini za kifashi kulingana na madhumuni mbalimbali yanayolengwa. Fasihi simulizi huwa na dhima ya kuizindua jamii kuhusu uhalisia wa maisha (Iribemwangi, 2013).

Chiragh'din (1974) anasema ya kwamba, wasichana wa Kiswahili walifundwa kama njia mojawapo ya kuwaandaa kwa shughuli za kijamii kama ndoa na malezi. Kulingana na (Gibbe, 1993) ufundaji huo ulikuwa sehemu ya kukuza taasubi ya kiume dhidi ya mwanamke. Ilikuwa ni njia ya kumfanya awe mnyenyekevu kwa mwanamume na jamii (Mulokozi, 1999). Ndalum and Kingé'i (1989) wanasema ya kwamba, fasihi simulizi ni hai zaidi ikilinganishwa na fasihi andishi. Fasihi simulizi ina mfungamano na maisha ya kila siku ya wanajamii na huonyesha tajriba yao ya kila siku (Wamitila, 2003).

Vitanzu vya fasihi simulizi huwa na lengo la kudhuhirisha hisia na maono ya wanajamii kuhusu masuala mbalimbali yanayowakumba. Shirikina za Kivumba zinagusia maisha ya unyumba, jamii na malezi ya watoto katika jamii ya Kivumba. Zinafanya hivyo kupitia matumizi ya ishara mbalimbali kuashiria maana hizo. McKay (1975) anasema ya kwamba, ndoa ni asasi muhimu sana katika jamii ya Kivumba na masuala kama uzinzi wala talaka hayakuruhusiwa. Shirikina za Kivumba zinatumia ishara ya mwanamke na mlango kubainisha maana hizo. Matumizi husika hata hivyo yanaashiria kuwepo kwa taasubi katika jamii hiyo kutokana na kwamba, zipo kimya sana kuhusu hulka ya mwanamume. Mwanamke anawekewa vikwazo vingi huku mwanamume akiachiwa uhuru wa kula kila aina ya vyakula na pia kutohusishwa na uleaji wa mimba, kuzaliwa kwa mtoto na kumnyoosha kihulka. Majukumu yote anaachiwa mwanamke.

Shirikina za Kivumba zinatumia ishara za mwanamke mjamzito, mlango(ni), shimo la choo, nyufa, kupanda darini na kula aina ya samaki (fumi) ni baadhi tu ya stiari hizo. Stiari hizo zote zinaashiria maana mbalimbali. Kulingana na Barthes (1973) kila kitu ni ishara na ina maana. Ishara husika zinastahili kufasirika barabara ndiposa maana kamili iweze kubainika. Kijamii, mwanamke huchukuliwa kama kiumbe dhaifu (Gibbe, 1993). Kuna juhudi za kimaksudi kijamii kama inavyodhihirika kupitia shirikina za Kivumba kumwekea mwanamke vidhibiti ili kumdhalilisha dhidi ya mwanamume. Mwanamke anadhibitiwa vyakula samaki wa aina fulani na kukute katika maeneo fulani ya nyumba. Mwanamke wa Kivumba hawezi kula kiporo wala kuketi mlango. Pia haruhusiwi kupanda darini. Mwanamke wa Kivumba anatarajiwa kuwa mtiifu na kufuata kila kanuni anayowekewa na jamii bila fursa ya kuuliza maswali. Chowdhry (2000) analifasiri tukio la kumdhibiti mwanamke kama la kisaliti kutoka kwa jamii ya kiume katika kumdunisha mwanamke. Kama anavyosema Mbele (1985), kufasiri shirikina kwa kutumia vigezo vya sayansi na dini badala ya utamaduni unaozichipua ni udhaifu.

Sirikina na sayansi havihusiani kwani huwa ni masuala ya imani za jamii husika (Arege na Matei, 2005; Wamitila, 2003).

Mjadala wetu unalenga kuonyesha ya kwamba, shirikina za Kivumba ni njama ya kimakusudi ya kumdhibiti mwanamke ili azidi kuwa mtiifu kwa mumewe na jamii (Sanja, 2020). McKay (1975) anasisitiza ya kwamba, Wavumba walikuwa na miko kuhusu takribani masuala yote kuhusu maisha. Wamitila (2003) wanasema ya kwamba, shirikina zina wajibu wa kijamii wa kukataza masuala ambayo yana imani hasi kwa jamii zikiruhusiwa.

### **Msingi wa Nadharia ya Semiotiki**

Semiotiki inatokana na neno la Kigiriki seme (semeiotikos), lenye maana ya ishara kulingana na Chandler (2002). Semiotiki ni uchunguzi wa matumizi ya ishara mbalimbali katika matini za kifasihi na dhima zake katika ufasiri wa maana. Mwaasisi wa nadharia hii anakisiwa kuwa Ferdinand De Saussure (1857–1913). Kulingana naye, kila ishara ina kifasiri chake na ndicho kifasiriwa. Ishara inaweza kuwa tamko ama neno. Kwa mujibu wa wana semiotiki, ishara inaweza kuwasilisha ujumbe kupitia fahiwati zote kama kusikia, kunusa, kuona, kugusa na kuonja kupitia uashiraji. Peirce Peirce (1839–1914) alisema ya kwamba, ishara ni kitu chochote ambacho kinasimama kwa niaba ya kitu kingine. Ishara inaweza kubeba maana zaidi ya moja kulingana na Peirce. Kulingana naye, mantiki katika ishara hutegemea tajriba na maarifa ya jamii husika ili kuifasiri.

Kila ishara ina msingi inakotegemeza ili kufasirika kwake kuwezekane, yaani kueleweka na kukubalika. Maana zao hutokana na mazoea ya jamii pamoja na utamaduni wa jamii husika (Short, 2007).

Jakobson (1896) anabainisha kwamba, miundo ya lugha ambayo hutumika zaidi katika uwasilishaji wa tungo ni ya kiishara. Tamathali hizo zinaweza kuwa za aina mbili: kauli za kitaashira (metonomia) na kauli za ki-sitiari (kimafumbo-kitamathali). Ujumbe ambao huwasilishwa huwa si wa moja kwa moja bali huwa ni wa kitamathali. Ishara huwa na maana zaidi ambayo hutokana na uhusiano uliopo baina ya ishara na kinachoashiriwa (Eco, 1976).

Katika mjadala wetu, tumezingatia zaidi misimbo ya Barthes (1980). Barthes aliwasilisha mawazo yake ya semiotiki kwa kutumia misimbo (Barry, 2002). Kisemiotiki, kila ishara ina maana bayana na ya kidhahania. Mojawapo wa misimbo hiyo ni msimbo wa matukio. Msimbo huo pia huitwa msimbo wa vitendo ama usimulizi (Hawkes, 2003). Msimbo huo hulenga kufafanua mfuatano wa matukio katika masimulizi na maana zinazojikuza katika akili ya msomaji kuhusiana na hali na sifa za matini zenyewe na namna mfasiri anavyoishia kupata jibu (Alli, 2013). Kulingana na Maliki na wenzake (2014), tukio la sasa husababishwa na tukio la awali na kumwelekeza msomaji wa matini za kifasihi katika fasiri kamili ya maana kupitia ishara husika.

Barthes pia aliibua msimbo wa kihemenitiki (Wamitila, 2002; Scholes, 1985). Huhusu uibuaji wa ishara zinazoleta hali ya taharuki ndani ya msomaji wa matini

za kifasihi na kumlazimu msomaji wa matini za kifasihi kuuliza maswali yanayotaka majibu. Mara nyingi hali hiyo hujibainisha kwenye anwani za matini ama mwanzo wa matini husika na kumhusisha msomaji wa matini. Msimbo huo hutumiwa kuelezea matini za kifasihi ambazo si za moja kwa moja na ambazo huibua hali ya taharuki ndani ya msomaji na kumwacha akijiuliza majibu kwa maswali kadhaa. Matini hizo huwa na sifa tata kuzifasiri na huwa hazijafanuliwa ndani ya matini zenyewe zinazochunguzwa ama la, huwa zimedokezwa tu. Huwa ni kama maana iliyocheleweshwa kwa mujibu wa Barthes.

Aidha Barthes aliibua msimbo wa kiseme. Neno seme hutumiwa kuelezea mfumo wa ishara zenye maana ambazo zinaweza kufasirika tu kutokana na maarifa ya mfasiri kuhusiana na tajriba ya kijamii ambamo ishara husika zinachipukia (Hawkes, 2003). Ishara husika huwa zinafahamika kwa wanajamii katika utamaduni husika. Huwezesha ufafanuzi na uelezaji wa matukio, mandhari ama wahusika kulingana na yanayosimuliwa na namna inavyosimuliwa ili kufasiri maana lengwa (Barry, 2002; Selden, Widdow na Brooker, 2005).

Msimbo mwingine wa kisemiotiki aliouibua Barthes ni msimbo wa ki-ishara. Msimbo huu hutumiwa kurejelea mfumo wa ishara ambazo huashiria maana za ndani katika matini za kifasihi ambazo sio wazi kwa mchanganuzi wa matini. Yaani, ishara huwa na maana ya kijuuju na maana ya ndani ambayo ni sharti ifanuliwe ndiposa maana iliyoashiriwa ipate kufahamika na msomaji wa matini za kifasihi. Msimbo huo humsaidia msomaji wa matini za kifasihi kung'amua uhalisia wa maana zinazolengwa kutokana na ishara zilizotumika (Barry, 2002). Hueleza hisia na hali ya kisaikolojia ya mhusika ama matini zinazosomwa. Ishara inaweza kuwa ni kitu dhahiri, mazingira ama usemi fulani unaoashiria maana zaidi ama mbadala.

Barthes (1973) aliibua msimbo wa kirejelezi. Msimbo huu humwezesha msomaji wa matini za kifasihi kung'amua maana zisizo za kawaida katika matini na zinazotumia ishara za kijamii, mapisi, sayansi ama kitamaduni ili uashiraji wake upate kufahamika. Msimbo huu huangalia namna msomaji wa matini za fasihi huishia kupata maana ya ishara kupitia tajriba yake ya muda mrefu katika maarifa ya kijamii, mielekeo yake ama itikadi. Kulingana na Barthes (Barry, 2007), kila kazi ya fasihi ina sifa mahsusi na inaweza kufasirika tu vyema kulingana na ujuzi wa msomaji wa kufahamu kaida maalumu za utanzu anaouchunguza kutokana na maarifa ya kusoma matini za aina nyingi kwa kutumiataratibu zinazokubalika ili kazi husika ifasirike kikamilifu na kwa njia ya kukubalika. Kiashirii huweza kuwa kilekile bali kinachorejelewa kikawa kitu tofauti kabisa kulingana na utamaduni na tajriba ya maisha ya wanajamii husika. Hii ndiyo misimbo ya nadharia ya semiotiki iliyohusishwa katika makala hii.

### Mjadala na Matokeo

Mjadala wetu utajikita katika ufasiri wa ishara na maana katika shirikina za Kivumba. Mjadala utatumia mifano ya Kivumba iliyokusanywa kutoka nyanjani pekee.

### Ishara zinazotumia Sitiari ya Mwanamke

Shirikina nyingi za Kivumba zinatumia ishara ya mwanamke katika mazingira mbalimbali zinazoashiria kuwepo kwa taasubi katika jamii husika. Mwanamke anasawiriwa akiwa mjamzito na mnyonge na wala hasitiriwi na jamii. Barthes (1968) anasema ya kwamba, kila kitu ni ishara na kina maana zaidi ya ishara yenyewe (Atkin, 2006). Ishara za mwanamke katika jamii ya Kivumba zinazoashiria taasubi ni pamoja na mwanamke akiwa na ujauzito.

### Ishara ya Mwanamke na Shimo la Choo/Nyufa

Katika muktadha wa Kivumba, tundu(ni) katika shirikina husika inaashiria shimo la choo.

*Mjamziro kachungulii tunduni, mroro akizaa achagherea kila akirudi:*

*Mjamzito asichungulie ndani ya shimo la choo (tunduni).*

Ishara ya ujauzito na mtoto kurejelea matendo na hulka ya mama yake ni ishara ya athari kumwachia mwanamke majukumu yote ya kulea na kumwadilisha mtoto huku mwanamume akiachwa bila majukumu yoyote kifamilia. Kulingana na shirikina hiyo, pale ambapo mtoto anapotoka ama hulka yake inakuwa na kasoro, mama ya mtoto ndiye wa kulaumiwa. Huu ni mtego ambao mwanamke wa Kivumba amewekewa na jamii yake (Sanja, 2020). Hali hiyo inaashiria ukosefu wa uhuru kwa jinsia ya kiume katika jamii ya Kivumba. Kulingana na nadharia ya semiotiki, tundu(ni) ni ishara ya hulka mbaya na mwanamke mjamzito anastahili kuiepuka (Sanders, 1977). Hali hiyo inaibua maswali mengi: mwanamke mwema wa Kivumba anastahili kuwa ana tabia na hulka gani? Nafasi ya mwanamume wa Kivumba katika kulea mimba hadi kuzaliwa kwa mtoto ni gani? Momanyi (2001) anakubaliana na Dollahite (2004) anaposema kwamba, jamii ina upendeleo dhidi ya mwanamke. McKay (1975) anatilia mkazo zaidi suala la taasubi anaponukuu Kipitu katika Ushairi wa *Kipitu* (ushairi wa Kivumba) :

*Mwanaruga na maere.*

Maana ya kijuujuu ya usemi huo ni kwamba, mwanamke wa Kivumba ana jukumu la kudumisha ndoa na kuvumilia kila kadhia ili isije ikavurugika na kuvunjika. Hakuna lawama inayomwendea mwanamume katika suala nzima la udumishaji wa ndoa. Ni dhahiri ya kwamba, katika jamii ya Kivumba, taasubi ya kiume dhidi ya mwanamke ni suala la kawaida. Kulingana na nadharia ya semiotiki (Barthes, 1977; Atkin, 2006), kurejeshwa kwa wazazi ni ishara ya talaka. Kulingana na (Maitaria, 2012) lugha ya kitamathali huwa na maana nzito na hulenga kuikoleza lugha. Hata hivyo, mara nyingi fasiri kamili hutegemea tajriba

ya mfasiri wa ishara kutokana na tajriba yake na maarifa ya muda mrefu kuhusiana na ishara husika.

### **Ishara ya Mwanamke Mjamzito na Kiporo**

Shirikina za Kivumba zinadhibiti kile mwanamke anastahili kula ama la huku mwanamume akiachwa huru kula atakavyo. Bila shaka hilo ni suala la taasubi ya kiume:

*Mjamziro kali mwiku: Mwanamke mjamzito asile kiporo*

Barthes (1977) aliibua msimbo wa kiseme. Msimbo huo hutumiwa kurejelea mfumo wa ishara ambazo huashiria maana za ndani katika matini za kifasihi ambazo sio wazi kwa mchanganuzi wa matini. Ishara ya mjamzito kula kiporo na kwenda msalani kuja na mtoto, ni ishara ya kujiathiri na kujitia aibu. Kiporo ni ishara ya suala lolote ambalo ijapo ni halali, mwanamke katika hali yake hatakiwi kujihusisha nalo. Ijapo kijuujuu ishara katika shirikina hiyo inaashiria ya kwamba, jamii inamlinda mwanamke, maana ya ndani inayoashiria kinyume na maana husika. Mwanamume hana vidhibiti. Katika mazingira ya kawaida, mwanamke anaweza kula kiporo bila kujali hali ya kimaumbile. Shirikina za Kivumba ni njama ya jamii ya kumfanya mwanamke kuonekana mnyonge. Kipora aidha kinaashiria ya kwamba, mwanamke ni mvivu na anapenda kulaza damu. Mulokozi (1999) anasema ya kwamba, utamaduni humfundisha mwanamke kuheshimu maadili ya kijamii na mikatale yake bila ya kumpa fursa ya kuuliza uhalali wa kufanya hivyo. Katika jamii ya Kivumba, inaonekana imani zinazotokana na shirikina huwa haziulizwi maswali.

### **Ishara ya Mwanamke na Ulaji wa Samaki**

Msisitizo kupitia shirikina za Kivumba ya kwamba mwanamke asile fumi mbali na kiporo zinaashiria kuwepo kwa taasubi na njama ya kuhini mwanamke.

*Mjamzito asile fumi: Mwanamke asile fumi*

Barthes (1973) aliibua msimbo wa kirejelezi. Msimbo huu humwezesha msomaji wa matini ya kifasihi kung'amua maana zisizo za kawaida katika matini na zinazotumia ishara za kijamii, mapisi, sayansi ama kitamaduni ili uashiraji wake upate kufahamika. Msimbo huu huangalia namna msomaji wa matini za fasihi huishia kupata maana ya ishara kupitia tajriba yake ya muda mrefu katika maarifa ya kijamii, mielekeo yake ama itikadi. Fumi ni ishara ya vyakula na masuala ambayo yanamwekea mwanamke vikwazo. Shirikina husika zinathibitisha kauli za (Chiraghdin, 1974) ya kwamba, mwanamke wa Kiswahili alifundwa kimakusudi kama njia ya kumweka chini ya mwanamume na jamii. Jamii badala ya kumlinda mwanamke, inamdhalilisha kwa kumwekea vikwazo. Kumnyima mwanamke wa Kivumba vyakula muhimu kama samaki ambayo ni muhimu kwa afya yake na mtoto aliyeko tumboni bila kumpa pendekezo mbadala ni ishara ya ubaguzi na ubinafsi dhidi ya jinsia yake.

### **Ishara zinazotumia Mlango(ni)**

Iribemwangi (2013) anadadisi ya kwamba, utamaduni ni tajriba ya ustaraabu wa wabajamii kuhusu kile wanachokiamini na mwonoulimwengu wao. Utamaduni humpa mwanajamii kitambulisho.

### **Mazingira ya Mwanamke Kuketi**

Mwanamke mjamzito wa Kivumba hana uhuru wa kuketi popote anapotaka na hasa mlangoni bila jamii kumwamulia. Hali hii inajibainisha sana kupitia mifano ya shirikina za Kivumba. Katika mifano tunasoma:

*Mjamziro kaka izungirini: Mwanamke mjamzito hatakiwi kuketi mlango (ni).*

Kisemiotiki, ujauzito ni ishara ya rutuba ya mwanamke na uendelezaji wa kizazi. Hiyo ndiyo sababu ya kumlinda mwanamke dhidi ya hatari zozote ambazo zinaweza kumdhuru yeye mwenyewe na pia mtoto. Mlango (ni) inaashiria chochote ambacho kinaweza kumtia hatarini na kuathiri afya yake na ile ya mtoto (Barthes, 1977). Hegedon (1983) anafafanua ya kwamba, ndoa ni muhimu sana na ni wajibu wa mwanamke na mwanamume na sio wa mmoja. Hali hiyo ni kinyume katika jamii ya Kivumba. Kumnyima kula fumi ni ishara ya taasubi ya kiume.

### **Mwanamke na Malezi ya Mtoto**

Utamaduni humpa mwanajamii kitambulisho (Iribemwangi, 2013). Maana katika vitanzu vya fasihi simulizi kama vipera vya shirikina huashiria jumla ya maarifa ya maisha yao ya kila siku. Hata hivyo, inaelekea utamaduni umetumiwa kama kisingizio tu. Hayo ni bayana katika shirikina kama:

*Ukaka kizingirini ukawa na mjamziro mroro pia ajakaa kizingirini: Ukiwa mjamzito uketi mlangoni ukijifungua na mtoto ataketi papo hapo*

Barthes aliibua msimbo wa kiishara (Barthes, 1973; Barry, 2002). Hueleza hisia na hali ya kisaikolojia ya mhusika ama matini zinazosomwa. Mtoto kuiga tabia za mama mzazi ni ishara ya mwanamke wa Kivumba kushindwa katika majukumu yake ya uzazi. Shirikina husika inaashiria na kusesitiza dhima ya mama wa Kivumba katika malezi ya mtoto. Hapana nafasi ya mwanamume katika mifano yote ya shirikina za Kivumba kuhusiana na suala husika. Shirikina hiyo inaashiria uhalisia kuwa, ijapo Wavumba wanaonyesha kumjali mwanamke kwa kumwekea ulinzi, hali ni kinyume.

### **Maudhui yanaoashiria Taasubi**

Kuna maudhui katika shirikina za Kivumba yanayoashiria taasubi kutokana na ufasiri wa ishara mbalimbali zilizotumiwa. Mfano wa ishara hizo ni muda ambapo mtoto anatakiwa kuwa nje ya nyumba. Ni majukumu ambayo bado yanasalia katika mikono ya mwanamke wa Kivumba pekee.

### **Mwanamke na Majukumu ya Afya ya Mtoto**

Chiraghdin (1974) anasema ya kwamba ndoa za wapwani ni za kuukeni na shirikina za Kivumba zinaashiria jibu husika. Mwanamume hahusiki moja kwa moja katika malezi ya mtoto na hilo linafanya watoto kuwa wa mama zaidi kuliko kuwa wa baba (Amana, 1982).

*Ukaka kizingirini ukawa na mimba mroro pia ajaka kizingirini: Ukiketi mlangoni ukiwa mjamzito ukijifungua mtoto naye atakuja kuketi mlangoni*

Msimbo wa kirerejelezi ambao Barthes aliibua unahusiana na namna msomaji wa matini anatumia maarifa yake ya muda mrefu kufafanua ishara ambazo zinamwegemeo wa kijamii (Maliki na wengine 2014). Mwanamume wa Kivumba hana majukumu kamili kama baba na mume kwa mkewe kutokana na kutokuwepo utaratibu kamili unaomjukumisha kijamii kupitia shirikina za Kivumba. Ni dhahiri mwanamume wa Kivumba hana mamalaka juu ya familia yake na huo ni udhaifu mkubwa kuhusiana na hali ya baadaye ya ndoa ya Kivumba.

*Mwana mchanga asiviibwe baada ya magharibi: Mtoto mchanga asisafishwe jioni*

Shirikina hiyo inasisitiza dhima ya malezi na hulka ya mzazi wa kike katika jamii ya Kivumba. Hata hivyo inaashiria zaidi ya malezi. Kulingana na Barthes (1968), ishara huwa na maana zaidi ya ishara yenyewe. Magharibi ni ishara ya hali isiyokuwa shwati na inaashiria hatari nyingi ambazo zinaweza kumkabili mtoto kiafya. Kimya kuhusu nafasi ya mwanamume katika suala hili linalohusiana na afya ya mtoto ni ishara ya taasubi ya kiume kuhusiana na malezi katika jamii ya Kivumba. *Kizingiri* kwa Kivumba ni mlango. Mlango hapa ni ishara ya kuweka wazi ama hadharani mambo ambayo yanastahili kuwa siri ya ndani. Mimba ni ishara ya suala ambalo ni la kibinafsi na muhimu kwa mhusika na anastahili kulilinda kwa dhati. Ujauzito unaashiria umuhimu wa kujichunga na kusitiri vitu vya thamani ambavyo mtu anavyo ndani yake. Mtoto kurejelea yale ambayo mama yake aliyafanya ni ishara ya kuathiriana kitabia ama kihulka. Inahusu pia hulka ya mwanajamii yeyote yule ambaye ana majukumu ya kulinda jambo muhimu kwa niaba ya jamii nzima katika jamii ya Kivumba na wala sio suala la mwanamke na malezi pekee.

### **Hitimisho**

Katika makala haya, ni wazi kwamba kuna taasubi haswa ya kiume katika jamii ya Kivumba. Kuna kimya kikuu kuhusiana na hulka ya mwanamume katika shirikina kuhusu unyumba, kulea na kutunza mke akiwa na ujauzito pamoja na majukumu mengine. Mwanamke anaachiwa majukumu yote ya kulea mimba pekee. Mwanamume wa Kivumba amepewa uhuru wa kula chochote na kuketi mahali popote huku mwenzake wa kike akidhibitiwa. Kumsawiri mwanamke katika hali yake ya unyonge (ujauzito) ni ishara ya kumdhalilisha na uendelezaji wa taasubi ya kiume dhidi yake.



## Marejeleo

- Abedi, K. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Dar es Salaam: Eagle Press.
- Akaranga, S. na Ifedha, D. (1987). *Semi za Kiswahili: Maana na Matumizi*. Oxford: Oxford Unievrstity Press.
- Amana, B. (1982) *Malenga wa Vumba*. Nairobi: Oxford University Press.
- Arege, T. na Matei, A. (2005). *Kunga za Kiswahili 3: Kitabu cha Mwanafunzi*. Nairobi: Focus Publishers.
- Atkin, A. (2006). *Pierce's Theory of Signs*. Retrieved November 15, 2010, from Stanford Encyclopedia of Philosophy: <http://plato.stanford.edu/entries/pierce-semiotics/>
- Barthes, R. (1977) *Writing Degree Zero*. Hill and Wang. Reissue Edition. Amazon. (English version)
- Barthes, R. (1972). *Mythologies*. Farrah, Straus and Giroux. Amazon. (English version)
- Barthes, R. (2018). *The Death of the Author na Elements of Semiology*. Macart Libray.
- Barthes, R. (1990). *The Fashion Systems*. California: University of California Press.
- Barthes, R. (1975). *The Pleasure of the Text*. Hill and Wang. Rissue Edition.
- Eco, U. (1996). *A Theory of Semiotics*. Bloomington: Indiana University Press.
- Gibbe, A. G. (1993). *Women and the making of Swahili Literature. OSSSREA research Report*. Oxford: OUP.
- Gornick, V., & Barbara, K. (Eds.). (1971). *Women in Sexist Society – Studies in the Power & Powerlessness*. New York: Basic Books Inc. Publishers.
- Chacha, C. N. (1986). *Mazingira ya Mwanamke Katika Fasihi ya Kiswahili* : ROSA Msitika wa E. Kezilahabi. Mwamko na 3. Nairobi: Nairobi Universty Press.
- Chiraghdin, S. (1974). “Kiswahili Na Wenyewe” *Mulika* 6: 35-41
- Chowdhry, M. (2000). *Inter Religion Marriage. A success story*. [http://www.Boloji.com/index.cfm.?Md=ontent\\$ArtideID=2168](http://www.Boloji.com/index.cfm.?Md=ontent$ArtideID=2168)
- Iribemwangi, P. I. (2013) *Cultural Transfer from Europe and Asia to Africa. Evidence from Borrowed lexicon Adapted into Kiswahili. International Journal of Education & Research (IJER)*, 1(8), 111-124.
- Oha, O. (1997). Flora Nwapa and the Semiotic of the Woman of the Lake. In Ebele Eko, et al. (Eds.), *Calabar Studies in African Literature*. Calabar: University of Calabar Press.
- Omeh, N. O. (2012). *Animal Imagery and the Main Characters in J.P. Clark-103 ANSU Journal of Arts and Social Sciences Bekereremo's Song of a Goat*” in Ozo-Mekuri Ndimele (ed.), *Expression: Journal of English Language Teachers Association of Nigeria*, Vol. 1.no.2.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Msingi na Vipenge Vyake*. Nairobi. Phoenix Publisher.

Webstar, R. (1990). *Studying Literary Theory: An introduction*. London: Edward Arnorld.

Wellek, R. na Warren (1949). *Theory of Literature*. London. Jonathan Cape.